Troubleshooting

Kama ukikumbana na tatizo kutumia MNM?

1) Kuifunga MNM bila kusevu

Kipindi cha utoaji ushauri kupitia MNM kina weza kusimamishwa wakati wowote , kwa kuchagua back-key chini ya skrini ya simu

na kisha: **Ignore Changes**.

Utapoteza taarifa zote za ushauri na kuifunga MNM.



2) Ikiwa MNM itaonekana tofauti baada ya kuiwasha

Ukiona maandishi makubwa na hakuna picha, basi kuna kitu hakikwenda sawa wakati wa utoaji ushauri, nenda kwenye kitufe cha **Go To Start** na **Go to End** chini ya skrini,



Chagua: **Go to End,** na **Save Form and Exit** au, kama kwanza utapata maswali kadhaa kujibu chagua kitufe cha back-key na kisha Ignore changes (kama inavyoonekana hapo juu), kabla ujaanza utoaji ushauri mpya.

Kupata msaada

Ikiwa utakumbana na tatizo katika kutumia app ya **Maize-Nutrient-Manager**, wasilisha tatizo lako kwenye group ya WhatsApp na kisha uliza swali. Unaweza pia kumpigia/kutuma ujumbe kwa Mukoma Kilakila.

MNM-Tanzania
Whatsapp group

Mukoma Kilakila
0765105980

Tanzania Agricultural Research Institute
TARI-UYOLE
P.O.Box 400, Mbeya, Tanzania

in collaboration with
NWO-Wotro GCP4 Scaling readiness project
CCAFS - Crop Nutrient Gap project

Maize-Nutrient-Manager
Tanzania
Southern Highlands
Mbozi and Momba districts

Mwongozo wa mtumiaji

Maize-Nutrient-Manager

Ushauri mahsusi kwa wakulima wa mahindi

Maize-Nutrient-Manager (MNM) ginatoa ushauri wa juu ya utumiaji wa uwiano sawa wa viritubisho na matumizi ya mbolea kwa ajili ya shamba **moja**. Kutegemeana na hali pamoja na ukubwa wa shamba, na fedha mkulima atawekeza, ita mshauri juu ya aina ya mbolea na matumizi yake, kiasi, wakati gani na namna nzuri Zaidi ya kuweka shambani.

MNM inakupatia ushauri kutegemeana na aina tatu za taarifa:

1. **Vipimo vya shamba** – *Kwa kutumia GPS ya simu, MNM itapima shamba ambalo mkulima anapanga kupanda mahindi msimu huu;*
2. **Hali ya shamba** – *MNM itarekodi mteremko, landscape position, na hali ya udongo ya shamba;*
3. **Usimamizi wa shamba** – *MNM itarekodi taarifa za shamba , kama vile mazao ya nyuma, aina ya mbolea na kiasi kilichotumika, wakati wa uwekaji na mavuno yaliyopatikana.*

Taarifa hizi hutumika ili kumpatia mkulima **ushauri mahsusi wa shamba** unaotegemeana na hali ya shamba lake na uwezo wake wa kiuchimi/fedha.

Nyenzo ya ujifunzaji

MNM ni *app* ya simu ambayo haijakamilika bado (kuwa katika mfumo ambao unaweza kupakua toka google play nk), lakini ni nyenzo kwaajili ya kujifunza. Kwa kurekodi kile ambacho wakulima mbalimbali wanafanya pamoja na mavuno yao, tunaweza kujifunza namna ya kuboresha ushauri na namna nzuri zaidi ya kuufikisha kwa wakulima.

Namna nyenzo app inavyofanya kazi

Toka **Start** hadi **Save Form and Exit**

Utawasha MNM toka home screen, kwa kuchagua:

MNM_Tanzania2020

Mara tu ya kuanza kutoa ushauri, kinachofuata ni kujibu tuu maswali katika skrini ukiwa Pamoja na mkulima – unamuhoji mkulima kwa kutumia app ya MNM. Baada ya kujibu swali, app itakupeleka kwenye swali linalofuata. Wakati Fulani inakulazimu kuchagua:

Endelea / Continue →

Mara zote unaweza kurudi nyuma kwenye swali lililopita katika app (kusahihisha majibu na kuchagua chaguo jingine) kwa kupangusa skrini kwenda kulia.

Kila mara unapomaliza kutoa ushauri, unachagua:

Save Form and Exit:



Hii ni skrini ya mwisho ya kila umalizapo ushauri. Ni pale tu unapobonyeza Save Form and Exit (ambayo pia huifunga MNM app), unaweza kuanzisha ushauri mpya kwa shamba jingine na mkulima mwingine. Unaweza kuwasha MNM tena kutokea skrini ya kwanza ya simu yako.

Badili lugha wakati wowote!

MNM ipo katika lugha ya Kiswahili *na* Kingereza

Unaweza kubadili lugha wakati wowote ukiwa unatumia MNM. Katika skrini yoyote uliopo, kona ya juu kulia, unaweza chagua: ⋮

Kisha chagua '**Change language**', na chagua:



Unaweza kurudi katika lugha ya awali kwa kufanya hivyohivyo!

Fomu za ushauri za Mkulima

Uandikaji ushauri wa MNM kwaajili ya mkulima

Wakati wa utoaji ushauri, **MNM** itakuambia wakati gani wa kuandika taarifa (ushauri) kwenye **Fomu ya Mkulima.** Utaona maandishi ya blue:

NAKILI USHAURI HUU KWENYE FOMU YA USHAURI

Mwachie mkulima fomu ya ushauri na mwambie aweke kumbukumbu ya kila anachokifanya katika shamba lake la mahindi kwa msimu wote, kama *vile aina na kiasi cha mbolea alichotumia (kg), wakati aliweka, palizi nk.*

Mwambie mkulima aangalie ikiwa mahindi katika shamba lake la MNM lina upungufu wa P na K, kwa kutumia picha zilizoko katika fomu.

Upimaji wa eneo lililovunwa

Kwa wakulima walioshauriwa na MNM & mashamba ya mahindi

Wakulima waliopata ushauri wa MNM msimu uliopita, na wale waliopanda mahindi katika mashamba wanayotaka kushauriwa na MNM; kwanza wataombwa kupimiwa eneo lililovunwa, amabalo ni eneo la shamba ambalo mkulima alipanda mahindi mwaka 2019.

> ***Zingatia!*** *Eneo lilivunwa mahindi linaweza kuwa dogo kuliko shamba lote, au kubwa/dogo kuliko eneo lililopimwa msimu uliopita.*

UVUNAJI:



Baada ya kupima eneoshamba la mahindi lililovunwa kwa msimu ulipita wa MNM (2019-20), mkulima ataulizwa kuhusu idadi ya magunia ya mahindi aliyopata kwa msimu huo ulipita.

Kisha jaza kiasi hicho cha mavuno (idadi ya magunia ya ujazo wa kilo 110/debe 6) na nyenzo MNM itakokotoa kiwango cha uzalishaji wa shamba hilo la mahindi.

Baada ya kupima eneo lililovunwa pamoja na idadi ya magunia kwa mwaka uliopita, MNM itatoa ushauri mpya kwa shamba hilo au jingine

Upimaji eneo la kupandwa

Kwa ushauri mpya wa MNM

Ikiwa mkulima anataka ushauri wa MNM kwaajili ya shamba lake la mahindi, nyenzo itamtaka kupima eneo la shamba hilo atakalo panda mahindi.

MNM itapima eneo hilo la shamba ambalo litapandwa mahindi msimu huu wa 2020-2021.

KUPANDA:



Tanzania Agricultural Research Institute
TARI-UYOLE
P.O.Box 400, Mbeya, Tanzania

in collaboration with
NWO-Wotro GCP4 Scaling readiness project
CCAFS - Crop Nutrient Gap project

Maize-Nutrient-Manager Tanzania

Southern Highlands

UPIMAJI SHAMBA Kutumia GPS ya simu

Upimaji eneo la shamba kutumia Maize-Nutrient-Manager

Kujua kiwango cha uzalishaji (mavuno) cha shamba hilo na kukadiria kiasi cha mbolea na mbegu zinazohitajika, ni lazima ukubwa wa shamba hilo ujulikane. Hivyo **Maize-Nutrient-Manager (MNM)** hutumia GPS ya simu kupima eneo hilo la shamba.

Kuifanya GPS ya simu ifanye kazi

Wakati wa kutumia MNM shambani, hakikisha simu yako ina chaji ya kutosha. Wakati wa kuanza kutoa ushauri kutumia MNM. Washa GPS ya simu, kwa kufanya yafuatayo:

(1) Pangusa skrini ya simu yako toka juu kuja chini;

(2) Bonyeza kitufe cha 'Location' kwa sekundu 3

(3) Kisha washa: **Location**



(4) Kama italazimika, bonyeza: 'Locating method' na



(5) Kisha chagua: GPS only
(vinginevyo GPS haitafanya kazi vizuri shambani)

(6) Bonyeza mshale-wa kushoto kurudi nyuma



> ***Zingatia!***
> Pindi upatapo swali hili:
> **Improve location accuracy?**
> *Chagua:* DISAGREE

Sasa unaweza kutumia MNM pamoja na sehem zake zote.

(Baada ya kumaliza utoaji ushauri kutumia MNM, unaweza kuzima 'location' ili kutunza chaji ya simu yako)

Upimaji eneo la shamba: Kuandaa GPS kwaajili ya upimaji shamba

Upimaji shamba lililovunwa au litakalo pandwa mahindi, ni rahisi. MNM itakuonesha maelekezo. Hivi divyo utafanya:

(1) Telezesha kidole chini ya skrini,
Phone settings for field measuring na chagua:

(2) Kwenye skrini inayofuata, kona ya juu kulia, chagua:

(3) Skrini ya **'Input Method'** kama inavyoonekana hapa:



Automatic
5 seconds
10 meters

(4) Anza kutembea pembezoni mwa KINGO za eneo la shamba unalopima (tazama ukurasa unafuata);

(5) Kadiri utembeavyo, hakikisha kidole kinakuwa kwenye skrini ya simu. Hii itazuia skrini kuzima (ikizima vipimo vyako vinakosa usahihi)

(6) Katika kila kona ya eneo la shamba unalopima, simama kwa sekunde 5, kisha endelea;

(7) Ukirudi pale ulipoanzia kutepembea nenda chini ya skrini:

(8) Kisha chagua: ***Endelea / Continue →***